

DHIMA YA MIANZO NA MIISHO KATIKA NATHARI ZA WATOTO: MIFANO KUTOKA  
NATHARI ZA KISWAHILI NCHINI TANZANIA

Edith B. Lyimo

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

edithbalyimo@yahoo.co.uk

**Ikisiri**

Fasihi ya watoto ni fasihi ambayo walengwa wake wakuu ni watoto. Fasihi hii ina umuhimu katika jamii kwa sababu ina dhima mbalimbali. Pamoja na umuhimu wa fasihi ya watoto katika jamii, fasihi hii ilichelewa kutambuliwa katika nchi za Afrika na duniani kwa ujumla ikilinganishwa na fasihi nyingine. Matokeo yake ni kwamba, fasihi hii imekuwa nyuma sana katika nyanja mbalimbali hasa za kiutafiti na kiufundishaji. Ili kukabiliana na changamoto hizi na nyingine, watafiti mbalimbali wa fasihi ya watoto wamekuwa wakitoa wito wa kufanyika tafiti zaidi kuhusiana na fasihi hii. Ijapokuwa katika jamii kitu kinachohusiana na watoto huonekana ni kitu rahisi, kwa mujibu wa tafiti na maandiko mbalimbali, fasihi ya watoto inahitaji umakini mkubwa katika utungaji wake na uwasilishaji wake. Fasihi ya watoto hutofautiana na fasihi ya watu wazima kwa upande wa fani, hasa katika vipengele vya wahusika, lugha, muundo na mtindo. Makala hii inajadili mianzo na miisho katika nathari za watoto. Lengo kuu ni kubainisha kaida na dhima ya waandishi katika kutumia mianzo na miisho katika fasihi ya watoto. Ili kufikia lengo hilo, makala itafafanua dhana ya nathari, aina zake, mwingiliano wake na tofauti zake na mwisho itajadili mianzo na miisho ya nathari pamoja na dhima yake kupitia vitabu teule vya Kiswahili vya fasihi ya watoto.